# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI

**23 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI – TAREHE 23 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**119. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Daraja la Mto Juhe Kata ya Samunge.

**120. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kusajili Wanafunzi katika Shule ya Msingi ya Ushirika Kata ya Mpuguso iliyojengwa kwa nguvu za Wananchi.

## WIZARA YA NISHATI:

**121. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mkoa wa Mtwara utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

## WIZARA YA FEDHA:

**122. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini hasara na faida kwa Makampuni kutotekeleza Sheria ya kujiorodhesha kwenye Dar es Salaam *Stock Exchange.*

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**123. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, SIDO ina mpango gani kukopesha Wajasiriamali vifungashio kama mabenki yanavyokopesha fedha ili kuongeza ubora wa bidhaa.

**WIZARA YA MAJI:**

**124. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda Kata za Mwamashiga, Mbutu, Isakamaliwa, Kining'inila Mwamakona, Igurubi na Kinungu utakamilika.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**125. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kusafisha na kuweka uzio Uwanja wa Ndege Urambo kwa kuwa ni muhimu kwa Biashara ya Tumbaku na ni Uwanja wa dharura.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**126. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kwa nini Mabwawa ya Samaki yaliyopo Kata ya Kalemawe - Same yasikabidhiwe kwa Wananchi wa Kata hiyo.

**WIZARA YA KILIMO:**

**127. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuimarisha kilimo cha Alizeti katika Wilaya ya Kakonko.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**128. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kulipa Madeni ya Wazabuni hasa ya Polisi na Magereza.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**129. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wahitimu waliosoma katika Vyuo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata usajili ili kuajiriwa nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**23 APRILI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**